

# Utatu Mtakatifu

Na Mchg. Thomas Maumbuka

Mjadala wa fundisho la Utatu Mtakatifu ulianzishwa katika Mkutano uliofanyika katika mji wa Nikea, mwaka 325 Baada ta Kristo (BK) Chini ya usimamizi wa Mfalme Constantino wa Roma na kuhudhuriwa na Maaskofu wapatao 300 toka sehemu mbalimbali duniani.

Lengo la mkutano lilikuwa ni kujadili nafasi ya Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu katika Mungu mmoja, jambo ambalo lilikuwa utata kwa waumini. Agano la Kale linatoa maelezo machache kuhusu Utatu Mtakatifu, kwa sababu wakati huo mkazo mkubwa ulikuwa katika umoja wa Mungu.

Tunasoma: “Sikiliza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana mmoja” (Kumb 6:4). Tunaposema Mungu ni Utatu jambo hilo linaelezekaje kwa yule asiye amini? Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, hizi ni nafsi tatu za Mungu mmoja, na wala siyo miungu mitatu. Kwa Kiebrania, ambayo ni lugha ya asili iliyotumika katika Agano la Kale Mungu “Elohim” lipo katika wingi. Katika uwingi huo Mungu mmoja anaonekana kufanya kazi kwa pamoja na wakati huo huo kila nafsi moja ikiwa peke yake (unity in diversity).

Mafundisho ya Yesu Kristo yanaonyesha kwamba nafsi tatu za Utatu ni sawa kabisa nazo ni Mungu kamili. Hakuna nafsi iliyo na upungufu au iliyo na hali ya juu kuliko nyingine. Lakini katika kazi yake kuna tofauti, kama Neno la Mungu linavyosema: “Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; ... kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka” (Yoh. 5:30); na anasisitiza kuyafanya mapenzi yake Yeye aliyempeleka yaani Mungu (Waraka kwa Waebrania 10: 5 – 7).

Kwa hiyo, tunapozungumza Mungu katika nafsi tatu haimaanishi kwamba tunaye Mungu Baba ambaye ana mtoto (Mwana) na Roho Mtakatifu ambaye ni mtumishi mtakasaji anayelijenga Kanisa. Na kwa maelezo mengine tunaweza kusema Baba si Mwana na Mwana si Roho na Roho si Baba lakini Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu na Roho ni Mungu.

Hii haina maana kwamba Mungu wa Agano la Kale ni tofauti na yule wa Agano Jipya. Jambo jipya katika Agano Jipya ni ufunuo wa Utatu na wala si Utatu wenyewe; yaani mpango wa wokovu katika Yesu Kristo ambapo katika huo tunamwona Mungu akijifunua katika nafsi tofauti kwa nyakati tofauti; kama baba wakati wa uumbaji, kama Mwana kwa ajili ya ukombozi na kama Roho Mtakatifu mtakasaji na msaidizi.

Tunapoangalia katika uumbaji, kulikuwa na muungano usiowezekana kutenganishwa baina ya Mungu na nguvu iliyotoa uzima na Roho wa Mungu. Tunasoma: “Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake,” (Zaburi 33:6).

Katika ukombozi tunamuona Yesu pia kama ilivyoielezwa hapo juu akifanya kazi kwa ushirika na baba na baadaye tunamuona Roho akikamilisha kazi ya Yesu ya kuisimamia imani ya waamini. Hivyo basi, Utatu Mtakatifu ni chombo ambacho Mungu anakitumia kwa kutekeleza kazi yake kwa njia ya watu wake, wanapojijenga katika imani.

(Mchg. Thomas Efraim Maumbuka barua pepe: tmaumbuka@yahoo.com)